# Hali na Hadhi ya Mwanamke katika Fasihi ya Kiswahili

Willy Migodela & Abel Nyamahanga
Chuo Kikuu Katoliki Ruaha
migodela@hotmail.com

**Ikisiri**
Makala hii imechunguza hali na hadhi ya mwanamke kwa kurejelea riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo.* Data za msingi zilizotumika katika makala zilipatikana kwa mbinu ya usomaji makini. Mbinu ya uteuzi lengwa ilitumika kupata data za msingi kutoka katika riwaya teule. Uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa katika makala hii umeongozwa na nadharia ya Ufeministi. Matokeo katika makala hii yanaonesha kuwa mwanamke amebainishwa katika nafasi mbalimbali zinazohusu malezi, utoaji wa maamuzi, ulaghai na usaliti katika mapenzi na ndoa. Mtazamo hasi unaodokezwa kuhusu mwanamke unasababishwa na harakati za mwanaume zinazowabana na kuwatumbukiza wanawake kufikia hapo walipo. Makala hii inahitimisha kuwa jamii inatakiwa kuchukua hatua za msingi za kuondokana na jambo linalowadhalilisha na kuwafanya wanawake wapuuzwe na kutazamwa katika udhaifu. Mwanamke hana budi kujijengea misingi imara ya kujitegemeana kufanya shughuli halali zenye tija ili kuiendeleza na kuidumisha heshima anayostahili katika jamii na taifa lake.

**MAKALA HALISI**

**HISTORIA YA MAKALA**

**Kupokelewa:** 05 Agosti 2021

**Kurekebishwa:** 30 Sept. 2021

**Kukubaliwa:** 25 Oktoba 2021

**Kuchapishwa:** 08 Dis. 2021

ISSN: 2453 – 6016

Juzuu 7,

Toleo 2,

pp. 11 – 19.

**NUKUU:** Migodela, W., & Nyamahanga, A. (2021). Hali na Hadhi ya Mwanamke katika Fasihi ya Kiswahili. *Ruaha Journal of Arts and Social Sciences*, *7*(2), 11 – 19.

**Maneno Msingi:** Hali, Hadhi, Mwanamke, Ufeministi na Fasihi ya Kiswahili.

## Utangulizi

Suala la maisha na harakati za mwanamke limejadiliwa na kushughulikiwa kwa mitazamo na misukumo mbalimbali katika jamii kupitia kazi za kifasihi. Maisha ya binadamu yametazamwa katika ngazi zote za maisha yake tangu kuzaliwa, malezi, ndoa, uzee hadi kifo. Kila ngazi katika maisha ya binadamu ina mambo na majukumu yake (Rutto, 2015). Kila jamii ina vikwazo vyake, miiko yake na masharti yake yanayomwongoza binadamu. Kanuni za jamii humfunga binadamu na kuingilia matakwa na shughuli zake za kujinufaisha, kujitafutia furaha na kujiendeleza kimaisha na kimtazamo. Katika harakati hizo binadamu wana matatizo yao, matakwa yao na maslahi yao. Baadhi ya masuala yaliyochunguzwa katika makala hii kupitia

riwaya teule yanahusu jinsi jamii inavyomtazama mwanamke katika jitihada za kuyakabili maisha yake kwa kurejelea riwaya teule.

Mwanamke amekuwa akitazamwa kwa namna mbalimbali na waandishi wengi wa kazi za fasihi. Miaka mingi iliyopita mwanamke aliwekwa utawani hadi pale Wanaufeministi walipoanza harakati zao za kumkomboa kutoka katika wimbi la kuonewa na kunyanyaswa kutokana na mfumo dume katika miaka ya 1960. Waandishi mbalimbali wamemchora mwanamke kwa mitazamo na misimamo inayohitilafiana. Fakih (2017) amemchora mwanamke kama mtu asiyestahili kujikwamua dhidi ya mfumo dume uliotamalaki katika jamii nyingi hapa nchini na kwingineko barani Afrika. Pia, wapo wanaomuona mwanamke kama kiumbe mwenye uwezo mkubwa anayestahili kuwa na uhuru kama mwanaume.

Kwa muda mrefu mwanamke alitazamwa kama chombo dhaifu katika jamii. Kabla ya Uislamu barani Afrika inasemekana hadhi ya mwanamke ilikuwa chini kuliko ngamia. Mwanaume alikuwa akimthamini zaidi ngamia wake kuliko mwanamke au mkewe (Githuci, 2013). Anaendelea kueleza kwamba katika jamii za Bara la Hindi zilizokuwa zikiafuata mila ya Sati, mwanamke aliyefiwa na mumewe alizikwa naye ili kumsindikiza. Pia, katika baadhi ya jamii za Kiafrika mila kama hiyo ilikuwepo ambapo chifu alizikwa na msichana wa kati ya miaka 14 hadi 17 kwa imani ya kwamba atakwenda kumstarehesha huko aendako. Hali hii ilimfanya mwanamke atazamwe kama mtu asiyestahili heshima, utu na kuheshimiwa katika jamii.

Dini ni mojawapo ya vyombo vya kijamii vinavyomtazama mwanamke kama aliumbwa ili awe msaidizi wa mwanaume (Sanga, 2013). Mtazamo huo humfanya mwanaume amtawale na kummiliki kikamilifu. Mwanamke anaangukia katika jukumu linalomfanya awe mnyenyekevu mbele ya mwanaume. Masoud (2018) anasisitiza kuwa asasi za dini ni kama wakala wa utamaduni unaolenga kumdunisha mwanamke. Utamaduni ndiyo unaoweka alama na kanuni zinazozoeleka na kutumiwa na jamii na baadaye huota mizizi na kutumika kama sheria rasmi za jamii inayohusika. Sheria hizo zinajengwa katika mfumo wa kimila na zinaendelea kuonesha nafasi na majukumu ya mwanamke na mwanaume kwa uwiano unaohitilafiana.

Kijamii, mwanamke hutazamwa kama kiumbe asiye na uwezo wa kushiriki kwa dhati katika shughuli za kijamii. Katika nyanja nyingi, wanawake huonekana kuwa ni watu wa kuongozwa tu. Jambo hili si sahihi kwa sababu uwezo wa wanawake kiuongozi umenyamazishwa bila sababu za msingi. Suala hili linatokana na mfumo uliopo katika jamii unaomini kuwa mwanamke anaweza kuwa kiongozi imara kama wanaume au zaidi yake (African Gender Equality Index, 2015). Suala la wanawake huendelea kuwekwa nje na kuachwa nyuma katika masuala ya msingi ya kijamii na kimaendeleo kama ilivyo katika baadhi ya sekta kama vile za jeshi na dini halina budi kuchunguzwa kwa kina ili kutafutiwa suluhisho linalofaa kwa maslahi mapana na endelevu ya jamii ya binadamu.

Ann (2013) anamtazama mwanamke kama nguzo thabiti katika kukuza uchumi wa familia, jamii na taifa. Pia, anaongeza kuwa hakuna asiyefahamu kuwa mwanamke ni nguzo kuu ya uzalishaji mali na uchumi wa familia na taifa. Kumuelimisha mwanamke ni njia mojawapo ya kuiokoa jamii na taifa katika janga la umaskini. Aburima (2014) anamweleza Ngozi Okonjo kuwa ni miongoni mwa wanawake wenye taaluma ya masuala ya uchumi waliosaidia kwa kiasi kikubwa katika harakati za kukuza uchumi nchini Nigeria. Okonjo alifanya kazi katika mazingira wazi na imara yalisayoidia nchi yake kurejesha nyumbani fedha zilizofichwa na vigogo katika mataifa ya kigeni. Mwanamke anaendelea kuwekwa nyuma katika sekta mbalimbali za kijamii kutokana na kuwepo kwa sababu mbalimbali. Wanawake wanahamasishwa kusoma kwa bidii ili kujenga uelewa mpana unaolenga kuongeza fursa pana ya kupigania na kusimamia maendeleo ya jamii zao kikamilifu. Baadhi ya wazazi katika baadhi ya jamii wamekosa mwamko wa kuwawezesha na kuwasomesha binti zao. Huu ni wakati sahihi wa kuunda sheria zinazotekelezeka zinazolenga kupambana na kuondoa mianya inayomdhulumu mwanamke katika sekta zote za kijamii hapa nchini. Makala hii imechunguza mitazamo kuhusu hali ya mwanamke katika jamii kwa kurejelea riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*.

**Mbinu na Mwega wa Uhakiki Kinadharia**

Makala hii imechunguza mitazamo kuhusu hali ya mwanamke katika jamii kwa kurejelea riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*. Data za msingi zilikusanywa kwa mbinu ya usomaji wa nyaraka. Uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa uliongozwa na nadharia ya Ufeministi. Mtazamo wa Ufeministi una historia ndefu duniani kwa kuwa uliibua vuguvugu la kutaka kufuta kabisa suala la uonevu dhidi ya mwanamke. Agenda ya Ufeministi inalenga kumaliza utawala wa mwanamume dhidi ya mwanamke (Gichovi, 2016). Nadharia hii imetumika kuchunguza uhusiano uliopo baina ya mwanamke na mwanamume kwa kurejelea riwaya teule iliyobainishwa. Mtafiti alimchunguza mwandishi wa riwaya teule katika muktadha wake wa kawaida ili kujua mtazamo wake kuhusu mwanamke kwa kuwa andiko lake ndicho kiungo chake. Uchambuzi kuhusu mitazamo na hali ya mwanamke katika jamii uliwekwa katika ulimwengu wa kawaida na halisi ili kufanya uhakiki wa kina kwa kurejelea riwaya teule.

**Mitazamo Kuhusu Hali ya Mwanamke katika Riwaya Teule**

Katika riwaya teule, suala la harakati za wanawake linaangukia katika mikabala mbalimbali ya kijamii. Uko mkabala unaolitazama suala la harakati za wanawake kutetea haki zao kama sehemu tu ya fujo za dunia (Barbara, 1999). Mkabala mwingine unafikiri kwamba suala la ukombozi wa mwanamke ni ule uhuru wa kuweza kurudi nyumbani kutoka kazini, kukaa na kusoma gazeti, pamoja na kushiriki katika mijadala mizito baina yake na mwanaume. Mtazamo huu ni sehemu ya ule unaohusu usawa wa Kiafrika unatumia mbinu ya kuheshimiana kama kisingizio cha kuhalalisha kuonewa na kukandamizwa kwa mwanamke. Suala la kukandamizwa kwa mwanamke linatazamwa kwa wepesi na linarahisishwa bila kupewa mtazamo sahihi wa namna ya kulishugulikia. Jitihada za ukombozi hazina budi kuzingatia misingi ya ukweli wa kihistoria kuhusu harakati za ukombozi wa tabaka la wanyonge katika

jamii. Kwa kurejelea riwaya teule, mwanamke amechorwa kwa namna mbalimbali kama ilivyoelezwa katika sehemu inayofuata.

**Ulaghai katika Mapenzi**

Mwandishi katika riwaya hii amejadili suala la mapenzi na ndoa katika pande mbili tofauti. Kwanza, ameonesha namna suala la mapenzi linavyotumika kama mbinu mojawapo ya kitapeli. Mwandishi anaonesha namna baadhi ya watu wasio waaminifu wanaofanya utapeli wa kimapenzi kama mbinu ya mojawapo ya kujipatia kipato. Mwandishi anaonesha namna Vera alivyomlaghai Dennis ili amuoe, ingawa moyo wa upendo wa kweli haukuwapo kabisa. Vera alimwandikia barua Dennis akimsihi kuwa ujauzito alikuwa nao ni wake Dennis alipaswa kumuoa na kumfanya mkewe, ingawa aligundua kuwa alikuwa amemdanganya (uk. 68). Suala hili limeshamiri sana katika jamii nyingi kutokana na kukosekana kwa uaminifu baina ya vijana wa kike na wa kiume. Hali hii imekuwa ikiibua migogoro ambayo wakati mwingine inasababisha baadhi ya watoto kukataliwa na kukosa matunzo na malezi bora baina ya wazazi wote wawili. Baadhi ya watu hulitazama suala la kupata mimba nje ya ndoa ni kiashiria kimojawapo cha kuporomoka kwa maadili katika jamii za Kiafrika.

Pia, mwandishi ameonesha jinsi vijana wengi wanavyotumia uhuru wao vibaya. Kwa mfano, katika riwaya hii, Tumaini alikuwa akilala na wasichana mbalimbali kwa zamu. Uhuru huo hauna tija kimaadili na ni hatari kwa ustawi na uendelevu wa jamii na taifa kutokana na kutamalaki kwa maambukizi ya magonjwa mbalimbali yaliyopo katika jamii (Shule, 2004). Kwa kiasi kikubwa, uhuru huo ulisababishwa na mfumo wa matumizi mabaya ya fedha zilizotumika kama chambo cha kuwanasa wasichana. Hali hiyo ilisababisha wasichana kupata mimba zisizotarajiwa na kukosa matunzo na kutelekezwa na mwanaume. Kwa upande mwingine, kukosekana kwa uaminifu miongoni mwa wanandoa ni hatari, hasa katika kipindi hiki kilichotamalaki maradhi ya kuambukiza kama vile UKIMWI. Mwandishi anaonesha jinsi Tumaini alivyoishi kilaghai na Anastazia baada ya kuamua kuanzisha makazi ya kudumu huko Shinyanga (uk. 96). Hali hii inamfanya mwanamke kuonekana kama chombo cha starehe cha mwanaume.

**Kujimudu Kimaisha**

Suala la mapenzi yanayojengwa katika misingi ya kupata pesa yanasemekana kushamiri sana, hasa sehemu za mijini mikubwa katika mataifa mengi. Mfumo huo unasababishwa na mitindo ya maisha, hali na ugumu wa fursa za uchumi wa kimji (Oyeronke, 2005). Jambo hili linachangia baadhi ya vijana kutafuta njia mbadala za kujikimu kimaisha ambazo wakati mwingine sio sahihi. Katika riwaya hii, Fatuma alikuwa na tabia ya kutembea na wanaume ilimradi apate chochote; na alikuwa tayari kuachana mara moja na mwanaume aliyefilisika. Fatuma alikuwa amebobea katika shughuli hiyo na mwepesi kutambua na kumfahamu mwanaume mwenye pesa na asiye na pesa. Pia, alikuwa amejijengea uwezo wa kuwatoroka na kuwaadhibu wanaume waliojaribu kumdhulumu kimapenzi. Suala la mwanamke kujihusisha katika mapenzi ya kibiashara linatokana na hali ya uvivu, utegemezi na kutowajibika kikamilifu ili kujimudu kimaisha. Matokeo yake, vijana wengi hujiingiza katika

shughuli zisizo na tija kijamii na kitaifa ili kukidhi mahitaji yao. Hata hivyo, wapo wanawake wanaojiingiza katika ukahaba kutokana na tabia binafsi ambazo hazihusiani na masuala ya kibiashara.

Pia, suala umalaya kama sehemu ya kuporomoka kwa maadili ya kijamii lilivyoshamiri katika sehemu mbalimbali za nchi, hasa katika miji na sehemu za machimbo ya madini. Mwandishi anaonesha namna Hadija alivyofanya umalaya kwa kuhamahama kutoka mkoa mmoja kwenda mkoa mwingine. Hadija alikuwa na uzoefu mkubwa katika suala la umalaya. Alifanya kazi hiyo katika maeneo mbalimbali ya nchi kama vile Tanga, Dar es Salaam (Buguruni), Shinyanga (Mwadui), Mwanza, Kigoma, Kilimanjaro (Moshi) na Tabora (uk. 85). Mapenzi ya namna hiyo yanavuka mipaka ya kijiografia ya jamii moja kwenda jamii nyingine. Mzagao wa namna hiyo unaongeza kasi ya baadhi ya maradhi ya kuambukizi kama vile UKIMWI (Lyatuu, 2011). Jamii haina budi kuepuka hali ya umalaya kwa kujijenga katika misingi ya maadili yenye tija kwa maslahi mapana ya uendelevu wa jamii ya mwanadamu.

**Mgongano Baina ya Ukale na Usasa**

Katika jamii nyingi suala la mgongano wa kijamii kuhusu uhuru wa kuoa na kuolewa bado linaendelea kukua na kuimarika licha ya kuwepo mwamko wa kielimu unaosisitiza uhuru wa kufanya jambo lolote bila kuvunja sheria. Kwa upande wa uhuru wa kuoa na kuolewa unasababisha mivutano mbalimbali katika jamii nyingi hapa nchini. Katika riwaya teule, uhuru huo ndio uliosababisha Anastazia kumtoroka mzee Tembo na kwenda kuishi Shinyanga Mjini na Tumaini kwa kuwa ndiye aliyekuwa chaguo lake. Suala la wazazi kuingilia uhuru wa kuoa na kuolewa linazua mitafaruku katika jamii nyingi hapa nchini (Suwed, 2013). Baadhi ya wazazi wanaoendelea kudumisha mila na desturi za kale zinazolenga kuwachagulia wachumba. Msingi wa kufanyika kwa jambo hilo unatokana na mtazamo kuwa wazazi ndio wanaomjua mchumba aliyeimarika kimaadili na kimajukumu ili kumtunza vizuri mwenzi wake. Hata hivyo, katika kipindi hiki cha utandawazi vijana wengi hawalikubali suala la kuchaguliwa mume au mke, badala yake huchagua kwa kufuata vigezo vyao na matarajio yao ya kimaisha.

Msigano uliopo baina ya wazazi na watoto wao kuhusiana na suala la kuchaguliwa mke au mume umezua matatizo mengi. Mwandishi anaonesha uhuru wa Anastazia kumtoroka mzee Tembo na kuambatana na Tumaini aliyekuwa chaguo lake. Jitihada za Anastazia kumtoroka Tembo na kuambatana na Tumaini ni suala linalotoa mafunzo mbalimbali kwa jamii, hasa kuhusu namna Anastazia alivyoolewa na Tembo na sababu za kumtoroka. Wapo wasichana wanaofanya hivyo kutokana na tamaa zao ama baada ya matarajio yao ya kimaisha kukwama. Hata hivyo, wapo wanaofanya hivyo huenda kutokana na ndugu au jamaa zao kuwashinikiza na kuoa au kuolewa nao. Kwa namna hali ilivyo sasa, uhuru wa kuoa na kuolewa hauna budi kutazamwa kama fursa ya kuifanya jamii kuzisahihisha asasi za kijadi za kijamii ili ziendane na mahitaji halisi ya maisha ya jamii bila ubaguzi wa kijinsia.

**Kufanya Maamuzi**

Katika jamii nyingi wanawake wanatazamwa kama watu wasio na maamuzi katika familia zao kutokana na kuwepo kwa sababu mbalimbali. Nafasi ya mwanamke katika kufanya maamuzi na uwakilishi wake ni mdogo katika ngazi za kijamii na kiserikali, ingawa katiba ya mwaka 1977 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 1984 inatoa haki sawa, hasa katika kupiga kura na kutumikia umma sawa kati ya mwanawake na mwanaume (Mapunjo, 2014). Katika riwaya teule, mwandishi anaonesha kuwa licha ya kuwa mama yake Tumaini alijua kuwa mali alizoachiwa mwanae Tumaini kama urithi zitamuathiri kimaadili, lakini alishindwa kubatilisha maamuzi ya marehemu mume wake. Mama yake Tumaini anaeleza:

> … ni vizuri zaidi mtoto kurithi vitu kama hivyo, licha ya hekima na kumrithisha mtoto pesa ni kama taji la uovu. Baba yako alikataa kabisa; na kwa kuwa nilishindwa mawazo ya baba yako alipokuwa bado mzima, siwezi sasa kugeuza tamko lake (uk. 15).

Nukuu hii inaonesha namna mama Tumaini alivyoshindwa kufanya maamuzi kuhusu namna bora ya kumlea mtoto wake kulingana na maadili ya jamii. Mama Tumaini alikosa maamuzi kuhusiana na mambo ya msingi na yenye tija kuhusu malezi ya mtoto. Licha ya kuwa alikuwa anaelewa madhara ya kumrithisha mali mtoto wake aliendelea kufuata tamko la marehemu mume wake. Inawezekana jambo hilo linatokana na  kuimarika kwa asasi za kijamii zinazomtaka mwanamke aheshimu na kutii matakwa ya mumewe bila  kujali ubora na udhaifu wa matakwa yao. Baadhi ya sekta zinazotumika kama nyenzo ya kupora haki za mwanamke ni utamaduni, dini, siasa na ndoa (Kajeza, 2016). Kuimarika kwa taasisi hizo kumesababisha kunyamazishwa kwa mwanamke kwani hawezi kutetea haki zake za msingi katika ngazi ya familia na taifa.

**Mitindo ya Malezi**

Suala la maadili na malezi bora katika jamii nyingi linasisitizwa kuanzia ngazi ya familia na taifa kwa ujumla. Hata hivyo, wazazi hawana budi kushirikiana kwa hali na mali ili kuwalea, kuwakuza na kujenga vizazi vyao katika misingi imara ya kimaadili, pamoja na kuwamudu kimahitaji (Sungi, 2011). Riwaya teule imeonesha athari na nguvu za mvutano wa kiuchumi zinazoainisha matendo ya mtu na mtazamo wake wote. Mwandishi ameonesha namna Tumaini alivyodekezwa na wazazi wake kwa kupewa pesa zilizomkengeusha na kumpa jeuri na uwezo wa kufanya lolote kabla ya kufikia umri sahihi wa kumiliki pesa nyingi (uk. 12). Tumaini alijengewa uwezo mkubwa wa kumiliki pesa jambo lililomfanya aache shule baada ya kujitumbukiza katika ulevi na mapenzi. Wajibu wa wazazi ni kuwajenga watoto katika misingi imara na endelevu ya kimtazamo na kimaisha badala ya kuwadekeza na kuwalea chini ya kiwango cha maadili yanayopaswa kufuatwa katika jamii.

Licha ya kuwa mama yake Tumaini alielewa kuwa mali za urithi alizoachiwa Tumaini zitamchanganya na kumwangamiza, lakini alishindwa kufanya maamuzi sahihi ili kumnusuru mtoto wake. Tumaini alilelewa kama yai na kusifiwa sana kwa lolote

alilofanya lenye tija na lisilo na tija kwa familia na jamii yake. Hayo yote yalimjenga katika misingi mibovu ya kitabia na kimaadili. Jambo hili liliongezwa na vitabu vya kibwenyenye alivyosoma Tumaini huko shuleni. Vitabu hivyo vilivyomfanya aamini kuwa wanawake ni vyombo vya kutumiwa na wanaume ili kutimiza haja zao za mwili (uk. 11). Matokeo yake Tumaini aliweza kuwalaghai na kuwatia mimba wasichana na kuwasahau, akiwamo Leonila. Kimaadili, jambo hili halikubaliki katika muktadha wa Tanzania na Kiafrika kwa ujumla. Kwa kawaida, jukumu la malezi na usimamizi wa maadili ya kijamii halina budi kujengwa katika misingi imara inayoihusisha jamii nzima.

Pia, mwandishi anaonesha namna Tumaini alivyokuwa akiwanyanyasa watumishi wao wa ndani kwa kuwa alijengwa katika misingi ya tabia na malezi ya kudekezwa kutoka kwa wazazi wake. Licha ya ukorofi wa Tumaini kwa wafanyakazi wao, mama yake alimkingia kifua na kuwafokea waliofanyiwa fujo. Hali hii inaleta mitafaruku katika jamii, hasa kutokana na kuwepo kwa matabaka ya walionacho na wasionacho. Tumaini alifanya hivyo kutokana na nguvu za kiuchumi ambazo zilitazamwa kama msingi wa maendeleo, ubora na mamlaka (uk. 64). Uhusiano wa Tumaini na watumishi wao wa ndani uliendelea kudhoofika jambo ambalo halifai kwa ustawi na uendelevu wa familia. Aidha, wafanyakazi wa ndani wanapaswa kuheshimiwa na kutazamwa kama sehemu kamili ya familia inayohusika. Suala la malezi thabiti halina budi kujengwa katika misingi ya utamaduni unaozingatia maadili mema kwa manufaa ya jamii na taifa.

**Hitimisho**

Katika makala hii, mwanamke amebainishwa katika nafasi mbalimbali, hasa kuhusu malezi na maadili, utoaji wa maamuzi, ulaghai na usaliti katika mapenzi na ndoa. Mtazamo hasi unaodokezwa dhidi ya mwanamke unasababishwa na harakati za mwanaume zinazowabana na kuwatumbukiza wanawake kufikia hapo walipo. Jamii inatakiwa kuchukua hatua za msingi za kuondokana na jambo linalowadhalilisha na kuwafanya wanawake wapuuzwe na kutazamwa katika udhaifu. Mwanamke anapaswa kujijengea misingi imara ya kujitegemea, kufanya shughuli halali zenye tija, kujitunza na kujiheshimu ili kuiendeleza na kuidumisha heshima anayostahili katika jamii na taifa lake.

Kitaaluma, makala hii inapendekeza kuwa itakuwa vizuri kama waandishi wataendelea kuandika kazi zao zinazolenga kupunguza pengo la mwachano wa kimahusiano uliopo baina ya mwanamke na mwanaume katika jamii. Pia, wanapaswa kuandika kuhusu umuhimu na matokeo chanya yanayotokana na kuwepo kwa ushirikiano uliopo baina ya mwanamke na mwanaume katika jamii na taifa kwa ujumla. Waandishi hawapaswi kuendelea kuijenga jamii ya wanawake katika mtazamo hasi unaoangukia kumdhalilisha na kumtweza kwa ujumla wake. Mojawapo ya namna bora ya kuisaidia jamii ili kushirikiana na kushikamana ni kutumia wenzo uliofumbatwa na waandishi wa kazi za kifasihi kutimiza wajibu huo. Kwa kurejelea maandiko yao, jamii itabadilika kulingana na mahitaji ya wakati huu tulionao kwani suala la umoja na mshikamano kati ya mwanamke na mwanaume ni la msingi katika

ujenzi wa jamii na taifa. Jamii itapata mwamko wa elimu, harakati za serikali na taasisi zisizo za kiserikali kuendelea kupinga na kukemea hali yoyote inayonuia kumtazama mwanamke katika mtazamo hasi zitawasaidia wanawake kufanikisha wajibu wao katika jamii.

**Marejeleo**

Aburima, A. E. A. (2014). Kutathmini Nafasi ya Mwanamke katika Mashairi ya Kiswahili: Uchunguzi wa Mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Africa Gender Equality Index, (2015). *Empowering African Women: An Agenda for Action – African Development*. Bank Group: African Development Bank.

Ann, S. S. (2013). *Usasa na Usasa wa Kisasa katika Nyuso za Mwanamke ya Said A. Mohamed.* Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Fakih, S. (2017). Kutathimini Mabadiliko ya Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya *Utengano* na *Kamwe si Mbali Tena*: Utafiti Linganishi. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Gichovi, M. K. (2016). The Journey Motif in Women's Identity Formation in David Mulwa's Flee, Mama Flee. A Research of Masters in Literature, University of Nairobi.

Githuci. M. C. (2013). Ujagina wa Mwanamke katika Pango.Tasinifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kajeza, R. T. (2016). Usawiri wa Mwanamke katika Fasihi Andishi: Mifano Kutoka katika Riwaya ya *Machozi na Damu* ya E. Shigongo (2005). Tasinifu ya Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.

Kezilahabi, E. (1975). *Dunia Uwanja wa Fujo*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mapunjo, G. C. (2014). Usawiri wa Mwanamke Kama Kiongozi Katika Tamthiliya: Uchunguzi wa *Kivuli Kinaishi* na *Nguzo Mama*. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Massoud, H. S. (2018). Kutathmini Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya *Mfadhili*. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Oyeronke, O. (2005). *African Gender Studies*. New York: Palgrave MacMillan.

Ruto, M. C. (2015). Matatizo ya Mwanamke katika Kidagaa Kimemwozea na Nyuso za Mwanamke. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sanga, A. (2013). *Wanawake na Injili katika Ujasiriamali.* Dar es Salaam: Ujuzi Education Publishers Limited.

Shule, V. (2004).'Effective Video Film Reducing Young Womens Gender Violence and Other. HIV Risk Behaviours'. A Research of Master Degree, University of Dar es Salaam.

Sungi, N. A. (2011). Ruwaza ya Shujaa Mwanamke wa Kiutendi katika Jamii ya Wanyanyembe wa Tabora. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Suwed, A. A. (2013). Usawiri wa Mwanamke katika Filamu za Steven Kanumba. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.